FUNZO LA JUMLA;
MAPENZI YA MUNGU-MTU MMOJA,NJIA MOJA NA LENGO MOJA.

Ujumbe wa Kwanza

Kujazwa na Elimu Kamili Ya Mapenzi Ya Mungu

Maandiko: Waefeso 1:5, 9, 11; Ufunuo 4:11; Wakol 1:9; 4:12

I. Mapenzi ya Mungu ni matakwa ya Mungu;mapenzi ya Mungu ni kile ambacho mungu Anataka kukifanya–Waefeso 1:9.

II. Uradhi wa Mungu ni mapenzi ya Mungu, Uradhi wake umo ndani ya mapenzi yake,na kwa hivyo mapenzi yake huja kwanza–v5.

III. Mapenzi ya Mungu,ni dhamira ya Mungu ya kutekeleza kusudi Lake–v 11; 1 Kor 1:1.

IV. Mungu ni Mungu wa makusudio,akiwa, na mapenzi ya Uradhi wake ,na aliviumbe vitu vyote kwa ajili ya mapenzi Yake ili atimize na akamilishe kusudi Lake–Ufunuo 4:11; Waefeso 3:9-11:

A. Mapenzi ya Mungu ni tamaa ya moyo Wake,ya kuchangamana na mwanadamu,na utimizo wa mpango wake wa milele–Waefeso 1:5, 9, 11; 5:17.

B. Mapenzi ya Mungu ni kuupata mwili wa Kristo kuwa ukamilifu,na dhihirisho Lake–Warumi 12:2, 5; Waefeso 1:5, 9, 11, 22-23.

V. Wakolosai ni Kitabu kinachohusu mapenzi ya Mungu–1:9; 4:12:

A. Mapenzi ya Mungu ambayo yametajwa kwenye kitabu hiki si mapenzi yake katika mambo madogo madogo-ni mapenzi ya milele ya Mungu,mapenzi makuu ya Mungu.

B. Wakolosai kinafunua ni yapi mapenzi ya Mungu kulingana na tamaa ya moyo wake,nia Yake ulimwenguni kote,katika uumbaji,ukombozi,enzi ijayo,na katika milele yote.

VI. Tunahitaji kujazwa na elimu kamili ya Mapenzi ya Mungu–Wakolo 1:9:

A. Mapenzi ya Mungu katika 1:9 ni mapenzi Yake kuhusu kusudi Lake la milele,kuhusiana na uwekevu wake kumhusu Kristo–Waefeso 1:5, 9, 11.

B. Kujazwa na elimu kamili ya mapenzi ya Mungu ni kujazwa na ufunuo wa mpango wa Mungu,ili tujue kile ambacho Mungu anapanga kufanya humu ulimwenguni–Ufunuo 4:11:

1. Mpango wa Mungu ni kumfanya Kristo awe kila kitu katika uwekevu wa Mungu–Matayo 17:5; Wakolosai 1:15-18; 3:10-11.

2. Tunapofunuliwa mpango wa Mungu,tunafunguliwa njia ya kuwa na uzoefu wa Kristo– 2:16-17; 3:4, 15-16.

C. Mapenzi ya Mungu ni tumjue Kristo Aliye-Jumlika,kuwa na uzoefu wake ,na kumuishi kama uzima wetu– 1:9, 15-18; 3:4.

D. Matokeo ya kuenenda inavyostahili Bwana,ni kufikilia elimu kamili ya Mapenzi ya Mungu;mwenendo kama huu ni mwenendo wa kumuishi Kristo–1:19-20a.

VII. Tunahitaji kusimama wakomavu na kuthibika sana katika mapenzi ya Mungu–Wakolo 4:12.

Ujumbe wa Pili

Mtu mmoja-Kristo Aliye-Jumlika.

Maandiko: Wakolosai 1:9, 12, 15-18, 27; 2:2, 8-9, 16-17; 3:4, 10-11, 15

I. Mapenzi ya Mungu yamo Katika Kristo,yanazingatia Kristo, na ni kwa ajili ya Kristo;Kristo ni kila kitu katika mapenzi ya Mungu–1:9.

II. Krist Anayefunuliwa katika wakolosai ni Yule Aliye-jumlika,Krist ambaye ni mmpana,,Aliye wa kwanza,kina na mambo yote katika uwekevu wa Mungu–vv15-18, 27; 2:16-17; 3:4, 10-11:

A. Wakolosai Kinafunua Kristo Aliye-Jumlika-Aliye Mungu,Mwanadamu,na ukweli wa mambo yote mazuri ulimwenguni–2:9, 16-17.

B. Kwa Kristo kuwa mzaliwa wa Kwanza katika uumbaji wa kwanza,na uumbaji mpya ,inamaanisha ya kwamba yeye ndiye yule Aliye-Jumlika na Ni mmpana–1:15, 18.

C. Kristo ndiye wa kwanza katika mambo yote,Anayechukua nafasi ya kwanza katika mambo yote–Wakolo 1:18.

D. Kristo Aliye-Jumlika na Aliye-mmpana ndiye kina cha mambo yote,kati na mduara(circumference) wa uwekevu wa Mungu–Matt 17:5, Wakolo 1:15-27, Waefeso 1:10.

III. Mapenzi ya Mungu ni ya Kwamba Kristo Aliye-Jumlika na Aliye-mmpana awe sehemu yetu–Wakolo 1:9, 12:

A. Katika Wakolosai 1:9, mapenzi ya Mungu ni Kristo;mapenzi ya Mungu ni makuu kuhusiana na sisi kumjua,kuwa na uzoefu,,na kuishi Kristo Aliye-Jumlika na Aliye-mmpana.

B. Mapenzi ya Mungu ni ya Kwamba tumjue Kristo,tuwe na uzoefu wa Kristo,tumfurahie Kristo,tuloeshwe na Kristo,na Kristo Afanyike uzima wetu na mtu ndani mwetu–3:4.

IV. Kristo Aliye-jumlika na Aliye-mmpana anaishi ndani mwetu kama tumaini la Utukufu–Wakolosai 1:27.

V. Kristo Aliye-Jumlika na Aliye-mmpana ni uzima wetu–Wakolo 3:4:

A. Neno uzima wetu linaashiria ya kwamba tunafaa kuwa na uzoefu wa Kristo Aliye-Jumlika yule Aliye ukweli wa mambo yote mazuri ulimwenguni kote–2:16-17.

B. Kwa kuwa Kristo ni uzima wetu,yote Aliyo nayo,yote aliyoyafikilia na kupokea yanafanyika yetu ili tuyafurahie Warumi –8:34, 10.

VI. Kristo Aliye-Jumlika na Aliye-mmpana ndiye sehemu au kiungo pekee cha mtu mmoja mpya–Wakolo 3:10-11:

A. Ujazo wa Kanisa kama mtu mpya, ni Kristo pekee yake;katika mtu mmoja mpya kunayo nafasi ya Kristo pekee yake kwa sababu Yeye ni kila mtu na ako ndani ya kila mtu.

B. Katika Kanisa kama mtu mpya,tumo ndani mwa Kristo,katika Kristo,na hadi kwake Kristo,na tumesimama ndani mwa Kristo,kuwa dhihirisho la Mungu katika Kristo–1:16-17.

VII. Kristo Aliye -Jumlika na Aliye-mmpana ni sehemu yetu–v20, 3:15.

Ujumbe wa Tatu

Njia moja-Msalaba wa Kristo

Maandiko: Wakolosai 1:20-22; 2:11-15

I. Kristo,mtu wa kipekee,ako kinyume cha vitu vyote,na msalaba,njia ya kipekee,ni kinyume cha njia zote–Wakolo 1:20.

II. Mtu mmoja-Kristo-ndiye Kiini cha ulimwengu wote na njia moja- msalaba- ndio kiini cha utawala wa Mungu–1 Kor 2:2; 1:17-18, 23; Wakalatia 6:14:

A. Mungu hutawala kila kitu kwa njia ya msalaba na husuluhisha kila kitu kwa njia ya msalaba–Wakolo 1:20, 2:14-16.

B. Katika msalaba wa Kristo Mungu amesuluhisha vitu vyote vilivyo kinyume ulimwenguni,na angali anatawala kila kitu kwa njia ya msalaba–Waef 2:14-16.

III. Kitabu cha Wakolosai kinatufundisha ya kwamba katika Maisha ya Kanisa ,Kristo anafaa kuwa yote ndani ya wote;chochote ambacho si Kristo kinafaa kwenda kwa msalaba–1:18, 3:10-11:

A. Kupitia kwa msalaba hatufai kufanyika kingine chochote ,kuwa na chochote na tusianze kufanya chochote.

B. Tukihepa kazi ya msalaba,yote tuliyo,vyote tulivyo navyo,na yale ambayo twaweza kuyafanya,hufanyika mmbadala(Replacement) na Kristo–1 Kor 1:17-18, 23.

IV. "Na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba Wake;kwa yeye ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi,au vilivyo mbinguni"–Wakolo 1:20:

A. Kwa sababu ya maaasi ya shetani;malaika mkuu,na malaika wote waliyomfuata,mbingu zilichafuliwa;na kwa hivyo siyo tu vitu vilivyo duniani vinafaa kupatanishwa,bali pia vitu vilivyo mbinguni vilihitaji kupatanishwa–v20b.

B. Kama watenda dhambi tulihitaji ukombozi,na kama maadui tulihitaji upatanisho–v14, 21-22.

V. "Akisha kuifuta ile hati au maagizo yaliyoandikwa kutushtaki kwa hukumu zake,iliyokua na uadui kwetu;akaiondoa isiwepo tena,akaigongomea msalabani"–2:4:

A. *Hati au maagizo* inamaanisha sheria za utaratibu na mila zake,ambazo ni aina tofouti tofouti ya kuishi na kuabudu–Waefeso 2:15.

B. *Kutundika msalabani* inamaanisha kukomesha sheria za amri katika maagizo.

VI. "Akiisha kuzivua enzi na mamlaka na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri akishangilia katika msalaba huo" –2:15:

A. Matukio yanayohusu Kristo,Mungu,na malaika waovu wanaotawala na mamlaka zote waliletwa msalabani;kwa hivyo msalaba ulifanyika njia ya Mungu ya pekee,na ya milele–vv14-15:

1. Kwa kusulubishwa kwake Kristo alifanya kazi ya kuutimiza ukombozi,na Mungu Baba alikua anafanya kazi ya kuzihukumu dhambi na kuzitundika sheria pale msalabani–v14.
2. Wakati huo huo,nguvu za giza na mamlaka yake walikua wakijishugulisha na majaribio yao ya kupinga kazi ya Mungu na ya Kristo kwa karibu muno; na kwa hivyo kulikua na vita vikali pale msalabani.

B. Mungu kwa dhahiri alizivua tawala zote na mamlaka yote ya giza pale msalabani na Akaibuka mshindi,huku akiwaaibisha kabisa–v15.

Ujumbe wa Nne

Lengo Moja-Kanisa Kama Mwili wa Kristo

Maandiko: Wakolsai 1:18; 2:19, 3:15; 4:15-16

I. Kristo Ndiye Kichwa cha Mwili,Kanisa–Wakolosai 1:18c:

A. Lazima tuone ya kwamba kanisa ni mwili,kiumbe ambacho kimejawa na Mungu wa utatu ,na watu wake aliowachagua na kuwakomboa–Waefeso 1:22-23; 4:4-6.

B. Umuhimu wa kindani wakanisa ni Mwili;Bila Mwili Kanisa halina maana yoyote–1Kor 12:12, 27; 1:2.

C. Ni muhimu sana wote tutambue ya kwamba Kristo ndiye kichwa na ya kwamba sis tu viungo vya Mwili Wake Wakolo 1:8, 2:9; Waefeso 4:16-16:

1. Kuishi katika Mwili ni kuishi Pamoja na viungo vingine chini ya Kichwa.
2. Ili kuishi Maisha ya mwili,ni lazima wote tuwe chini ya Kichwa,na kisha tumchukue Kristo kuwa uzima wetu,Mtu wa pekee,na kiini katika maisha yetu.
3. Kanuni ya kwanza ya kuishi katika mwili wa Kristo,ni kuyatii mamlaka ya Kichwa-Kristo–Waefeso 4:15:
   a) Kristo ndiye kichwa cha mwili, na uzima unaweza kutiririka vizuri hadi ndani mwetu iwapo yeye ako uongozini kikamilifu–v16.
   b) Wajibu wa mwili kwa Kichwa ni utiifu na usikivu pasipo maoni,wazo,wala mapendekezo–Yohana 21:2022;Matendo 19:1-4a.

II. Mwili hukua kwa ukuaji wa Mungu–Wakolosai 2:19:

A. Ukuaji wa mwili hutegemea ukuaji wa Mungu,ongezeko la Mungu ndani mwetu–Waefeso 4:16.

B. Mungu hupeana ukuaji kwa kujipeana mwenyew ndani mwetu–3:16-17a:

1. Mungu kutupatia ukuaji kwa hakika inamaanisha Mungu anajipeana Mweneyewe kwetu–1 Kor 3:6-7.
2. Zaidi Mungu anavyoongezeka ndani mwetu ndivyo Zaidi anavyopeana ukuaji–Waefeso 4:15-16.

III. Katika Mwili mmoja tuliitiwa amani ya Kristo,ambayo Ndiye Kristo Mwenyewe-Wakolo 3:15:

A. Kwa kukomesha hati na maagizo yanayotenganisha katika mwili wake ,yaani,kuangamiza uadui,na kwa Yeye kuumba hawa wawili;Wayahudi na Wayunani kuwa mtu mmoja mpya,Alifanya amani kati ya waamini wote–Waefeso 2:15.

B. Kwa ajili ya Maisha ya mwili ,tunafaa kuruhusu amani ya Kristo iamue mambo yote mioyoni mwetu katika mahusiano yetu na wandugu wengine katika mwili–Wakolo 3:15.

IV. Kama viungo vya Mwili,tunahitaji kuwa na ufahamu wa Mwili na hisia za Mwili–1 Kor 12:25-26, Warumi 12:15:

A. Kama vile mtume paulo alivyokua ,na sharti kuchukua hisia ya kichwa kuwa hisia yetu wenyewe;Hili jambo linahitajika sana katika maisha ya Mwili–Waef 1:8.

B. Lolote tunalolifanya linahusu Mwili;na kwa hivyo katika jambo lolote tulifanyalo,ni sharti tuujali Mwili,huku tukichukua Mwili kuwa mwongozo katika nia zetu,mawazo,maneno,na matendo yetu–1 Kor 12:12-27, 2 Kor 8:21.

V. Mwili wa kipekee wa Kristo unadhihirishwa kama Makanisa ya miji–Wakolosai 4:15-16, Waefeso 4:4, Ufunuo 1:4, 11:

A. Mwili mmoja ndilo Kanisa moja la Mungu,likidhirishwa katika miji mingi kama Makanisa ya miji– Matt18:18; 18:17; Waefeso 1:22-23; 2:21-22; 1 Kor 1:2, 12:27

B. Kanisa la mahali ni dhihirisho la Mwili wa Kristo mahala hapo.–1 Kor 1:2; 10:32b, 17; 12:12-13, 20, 27.